SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Kumbukumbu Nam CA.16/306/01..... **26 July 2022**

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya Utumishi Serikalini inatangaza nafasi za kazi za ualimu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya Skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari Unguja na Pemba Kama ifuatavyo:-

1. MWALIMU "GRADE A" SANAA DARAJA LA II -ZPSF-10 Nafasi 29 Unguja na Pemba

Ufafanuzi wa nafasi hizo ni kama ifuatavyo:

MASOMO	IDADI
History-English	10
Geography- English	19
JUMLA	29

Sifa za waombaji.

Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka 46

Awe mwenye Shahada ya Kwanza ya Ualimu wa Sanaa katika tahsusi (combination) za masomo ya Geography- English au History-English kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapindizi ya Zanzibar.

Majukumu

i. Kufundisha katika Skuli za Sekondari
ii. Kutathmini maendeleo ya wanafunzi na kutoa taarifa kwa uongozi;
iii. Kutoa taarifa za tathmini hizo kwa uongozi wa skuli;
iv. Kutunga na kusahihisha mitihani ya wanafunzi.
v. Kuandaa kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi na kufuatilia mahudhurio ya wanafunzi.

vi. Kuandaa ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na ya mwaka;

2. MWALIMU "GRADE A" SAYANSI DARAJA LA II ZPSG-02. Nafasi 221 Unguja na Pemba

Ufafanuzi wa nafasi hizo ni kama ifuatavyo:

MASOMO	IDADI
Biology	20
Chemistry	20
Physics	80
Mathematics	100
Agricultural Science	1

Sifa za waombaji.

Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka 46

Awe mwenye Shahada ya Kwanza ya Ualimu wa Sayansi katika katika masomo ya Biology, Chemistry, Physics na Mathematics au Agricultural science kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapindizi ya Zanzibar.

Majukumu

i. Kufundisha katika Skuli za Sekondari
ii. Kutathmini maendeleo ya wanafunzi na kutoa taarifa kwa uongozi;
iii. Kutoa taarifa za tathmini hizo kwa uongozi wa skuli;
iv. Kutunga na kusahihisha mitihani ya wanafunzi.
v. Kuandaa kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi na kufuatilia mahudhurio ya wanafunzi.
vi. Kuandaa ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na ya mwaka;
vii. Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

3. MWALIMU "GRADE B" DARAJA LA III (ZPSD-06/SANAA) (ZPSD-08/SAYANSI) Nafasi 590 Unguja na Pemba

Ufafanuzi wa nafasi hizo ni kama ifuatavyo:

Nam.	WILAYA	IDADI YA NAFASI		JUMLA
		MASOMO YA SANAA	MASOMO YA SAYANSI	
1	Wilaya ya Wete	30	70	100
2	Wilaya ya Micheweni	30	70	100
3	Wilaya ya Mkoani	30	70	100
4	Wilaya ya Chakechake	50	50	100
5	Wilaya ya Kaskazini A	50	50	100
6	Wilaya ya Kati	40	40	80
7	Wilaya ya Kusini	5	5	10

Sifa za waombaji.

Awe Mzanzibari mwenye umri usizidi miaka 46

Awe na Stashahada ya Ualimu wa Msingi (Diploma in Primary Education) ya Sanaa/Sayansi, kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar.

Majukumu

i. Kufundisha Skuli za Msingi.
ii. Kutathmini maendeleo ya Wanafunzi.
iii. Kutoa taarifa za tathmini na matokeo mbali mbali kwa uongozi wa Skuli.
iv. Kujenga mashirikiano kati ya walimu, Wanafunzi na Wazazi au Walezi.
v. Kuandaa na kutunza kumbukumbu za maendeleo ya Wanafunzi.
vi. Kutoa ushauri nasaha kwa Wanafunzi, Wazazi na Walezi.
vii. Kutunga, kusimamia na kusahihisha mitihani Skuli katika ngazi anayofundisha.
viii. Kutathmini Mitaala ya masomo wanayofundisha.

3. MWALIMU "GRADE C" DARAJA LA III- ZPSC-06 Nafasi 488 Unguja na Pemba

Ufafanuzi wa nafasi hizo ni kama ifuatavyo:

Nam.	WILAYA	JUMLA
1	Wilaya ya Wete	70
2	Wilaya ya Micheweni	88
3	Wilaya ya Mkoani	50
4	Wilaya ya Chakechake	50
5	Wilaya ya Kaskazini A	40
6	Wilaya ya Kaskazini B	40
7	Wilaya ya Mjini	20
8	Wilaya ya Magharib A	30
9	Wilaya ya Magharib B	40
10	Wilaya ya Kati	40
11	Wilaya ya Kusini	20

Sifa za waombaji.

Awe Mzanzibari mwenye umri usiopungua miaka 46

Awe mwenye Cheti cha Ualimu wa Maandalinzi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Majukumu

i. Kufundisha Skuli za Maandalizi
ii. Kutathmini maendeleo ya Wanafunzi;
iii. Kutoa taarifa za tathmini hizo kwa uongozi wa Skuli;
iv. Kusahihisha mitihani ya Skuli na kitaifa katika ngazi ya Msingi.
v. Kuandaa na kutunza kumbukumbu za maendeleo ya Wanafunzi.
vi. Kujenga mazingira yanayofaa kufundishia/kujifunzia.
vii. Kuhimiza na kufuatilia mahudhurio ya Wanafunzi.
viii. Kusimamamia masula ya nidhamu ya Wanafunzi
ix. Kutunga, kusimamia na kusahihisha mitihani Skuli katika ngazi anayofundisha.
x. Kuandaa maazimio ya kazi na maandalio ya masomo.
xi. Kuweka kumbukumbu za kila siku za masomo anyofundisha;

xii. Kuandaa ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka;

Jinsi ya Kuomba*:*

- Maombi yote yatumwe kwenye **mfumo wa *Kielektronic wa ajira (Zanajira)*** kupitia anuani ifuatayo:- https://portal.zanajira.go.tz kuanzia tarehe 01 Agosti, 2022 hadi tarehe 21 Agosti, 2022

- Mfumo huo pia unapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini www.zanajira.go.tz

- Muombaji anatakiwa kuainisha nafasi ya kazi pamoja na Wilaya anayoiombea.

TANBIHI:

Tume ya Utumishi Serikalini inawatahadharisha waombaji wote kwamba ajira zinatolewa bure. Hivyo, wanatakiwa kujiepusha na Matapeli wanaotumia nafasi hizi kwa kujipatia kipato kisicho cha halali.